Washington State Department of Social & Health Services
Transforming lives

Chaguo lako la Kuchukua Msaada wa Malezi ya Mtoto ikiwa bado Unapokea Msaada wa Muda kwa Familia Maskini (TANF)

Ukipokea TANF kwa ajili ya watoto walio chini ya ulezi wako, lazima usaidie idara ya Huduma za Jamii na Afya (DSHS), Kitengo cha Msaada wa Malezi ya Watoto (DCS), kuchukua Msaada wa Malezi ya Mtoto ila tu isipokuwa salama kwako au watoto. Kitengo cha Huduma za Jamii (CSD) huamua kustahiki kwa TANF na kupendekeza kwa DCS kutoa huduma ya utekelezaji wa msaada kamili iwapo wewe au mtoto (au watoto) watapokea TANF Huduma hizi zinaweza kujumuisha kushurutisha wajibu wa mzazi mwingine kutoa bima ya afya na kuchangia mgawo wao wa gharama ya afya bila bima kwa mtoto (au watoto).

Ni nini nahitaji kufanya ili kusaidia DCS kukusanya msaada wa malezi kwa mtoto?

- Jina la mzazi (au wazazi) mtoto (au watoto).
- Tupatie taarifa ya ziada ili kusaidia kupata mzazi (au wazazi).
- Saidia kuhakiki ni nani mzazi (au wazazi) wa mtoto (au watoto).

Kuna umuhimu gani wa kuthibitisha baba mlezi na kupokea msaada wa malezi ya mtoto?

- Kwa sababu msaada wa malezi ya watoto unaweza kukusaidia kuthibitika kifedha.
- Kwa sababu inapatia mtoto (au watoto) historia ya kiafya ya familia wanapojua mzazi wao ni nani.
- Kwa sababu inapatia mtoto haki ya kisheria ya kurithi, usalama wa kijamii, faida wa wastaafu wa kijeshi na faida na haki nyinginezo za serikali.

Ni nini hufanyika nisiposhirikiana na DCS?

Ikiwa unapokea faida bila kusaidia DCS kukusanya msaada wa malezi ya mtoto, kifungu chako cha ruzuku ya pesa inaweza kupungua kwa asilimia 25. DCS itafuatilia makusanyiko ya msaada wa malezi ya mtoto bila ushirika wako.

Ni wakati upi *sio* sawa kushirikiana na DCS?

Sio lazima kukusanya msaada wa malezi ya mtoto ikiwa mhudumu wako wa CSD ataamua kuwa una nia njema kutosaidia. Sababu za Nia Njema ni:

- Unahofu kuwa wewe au watoto walio chini ya malezi yako watajeruhiwa kimwili au kiakili.
- Mtoto wako alizaliwa kutokana na ubakaji au kujamiiana kwa maharimu.
- Umeanzisha taratibu za kuasili au upo katika ushauri (kwa hadi miezi mitatu) na shirika la utaratibu la uasili wa watoto kuhusu uasili.

Ni nini nafaa kumpa mhudumu wangu wa CSD kuonyesha kuwa nina Nia Njema ya kutosaidia?

- Kauli yako iliyotiwa sahihi inayoeleza hofu na wasiwasi zako (ikijumuisha fomu hii) au
- Rekodi zozote ikiwa pamoja na za kimatibabu, polisi, kauli za jamaa na marafiki kuhusu madai yako ya usalama, ikiwa zinapatikana.
- Uko na siku 20 kutoa uthibitishaji huu lakini unaweza kuomba muda zaidi iwapo haja.

Je, naweza kuhakikisha msaada wa malezi ya watoto umekusanywa bila kushirikiana na DCS?

Ndio, kwa sababu kuna viwango viwili tofauti ambavyo unaweza kuchagua; Kiwango A au Kiwango B.

- Kiwango A: Hutaombwa kushirikiana na DCS. Msaada wa malezi ya mtoto hautakusanywa.
- Kiwango B: Hutaulizwa kushirikiana na DCS *lakini* msaada wa malezi ya mtoto utakusanywa na anwani yako itabakia kulindwa.

Nafaa kufanya nini ikiwa sio salama tena kwa DCS kukusanya Msaada wa malezi ya mtoto?

- Wasiliana na CSD na afisa wako wa msaada wa malezi ya watoto wa DCS mara moja. Waambie wote wawili kuhusu hali yako mpya.
- Tuma ombi la Nia Njema kwa kukamilisha fomu hii.
- Ikiwa bado upo na Nia Njema ya Kiwango B, zingatia kubadili hadi Kiwango A.
- Omba rufaa ya mashinani au kwa wakili wa vurugu za nyumbani katika jamii.

Nafaa kufanya nini nikitofautiana na maamuzi ya Nia Njema ya CSD?

Una haki ya kutuma ombi la Kusikilizwa kitawala kuhusu maamuzi ya Nia Njema.Kesi ya kusikilizwa kitawala ni kuangaliwa upya maamuzi ya Nia Njema. Tizama “Mchakato wa Kesi ya kusikilizwa kitawala” katika ukurasa wa mwisho ili upate taarifa zaidi kuhusu kisikilizwa kitawala.

Ikiwa una maswali yoyote kuhusu kusaidia na kukusanya msaada wa malezi ya watoto, uliza kabla ya kutia sahihi katika fomu hii. Chagua kauli moja tu kati ya hizi hapa chini.

☐ Naamini kuwa ni salama kwangu na watoto wangu kwa DCS kukusanya msaada wa malezi ya watoto. Naelewa kwamba lazima nisaidie DCS kukusanya msaada wa malezi ya watoto na nisipofanya hivyo, ruzuku yangu ya pesa itapunguzwa kwa asili mia 25.

☐ Nina sababu nzuri ya kutosaidia. Tafadhali eleza sababu yako ikiwa pamoja na hofu na wasiwasi zako kwenye ukurasa unaofuata.

Hali ya kila familia ni tofauti. Tafadhali chagua vijisaduku vyote ambavyo vinaeleza kwa nini inaweza kosa kuwa salama kufuatilia msaada wa malezi ya mtoto.

- ☐ Mtoto (au Watoto) wanahusika na taratibu za kisheria za uasili.
- ☐ Mtoto (au watoto) walizaliwa kutokana na ubakaji au kujamiiana kwa maharimu.
- ☐ Nina agizo la kuzuia au ripoti za polisi kwa mzazi asiyekubaliwa kisheria kuishi na mtoto kisheria.
- ☐ Mzazi asiyekubaliwa kisheria kuishi na mtoto amejeruhi au kutishia kunidhuru mimi au mtoto (watoto).
- ☐ Mzazi asiyekubaliwa kisheria kuishi na mtoto ana historia ya tabia za vurugu.
- ☐ Mzazi asiyekubaliwa kisheria kuishi na mtoto atajaribu kutwaa mtoto (watoto) ili kuishi nao ikiwa msaada wa malezi ya mtoto utafuatiliwa na hii itapokonya mtoto (watoto) mazingira salama.
- ☐ Nina wasiwasi kuwa uthabiti wa mtoto (au watoto) utavurugwa.
- ☐ Ikiwa msaada wa malezi ya mtoto utafuatiliwa, mzazi asiyekubaliwa kisheria kuishi na mtoto anaweza kuleta vurugu na kusababisha kuumia kiakili kwa mtoto (au watoto).
- ☐ Mzazi asiyeruhusiwa kisheria kuishi na mtoto ana changamoto za afya ya kiakili na ulanguzi wa madawa ya kulevya ambazo zinaweza kunidhuru mimi au mtoto (watoto).
- ☐ Nyinginezo, tafadhali eleza hofu na wasiwasi zako hapa chini:

Nakiri kwamba taarifa ya hapa juu ni ya ukweli.

JINA LA MTEJA (KWA HERUFI KUBWA)	NAMBARI YA KITAMBULISHO CHA MTEJA
SAHIHI YA MTEJA	TAREHE

Nimepatia mteja nakala ya fomu hii.

SAHIHI YA MHUDUMU	TAREHE
JINA LA MZAZI ASIYERUHUSIWA KISHERIA KUISHI NA MTOTO	NAMBARI YA KITAMBULISHO CHA MTEJA
JINA LA MTOTO	NAMBARI YA KITAMBULISHO CHA MTEJA
JINA LA MTOTO	NAMBARI YA KITAMBULISHO CHA MTEJA
JINA LA MTOTO	NAMBARI YA KITAMBULISHO CHA MTEJA

Mchakato wa Kesi ya Kusikilizwa Kitawala

1. Kwa uhakiki wa kesi yako, pigia CSD kwa 1-877-501-2233.
2. Kutuma ombi la kusikilizwa kitawala wasiliana na CSD au andikia Ofisi ya Kesi za Kusikilizwa Kitawala, PO Box 42489, Olympia, WA 98504-2489 katika siku 90. DCS haitaanza kushughulikia kesi yako hadi maamuzi ya kusikilizwa yatakapohitimishwa.

   Mwanasheria au mtu mwingine anaweza kukuwakilisha katika kusikizwa kwa kesi yako au unaweza kujiwakilisha

Je, ninaweza kupokea ushauri wa kisheria au kuwakilishwa?

Unaweza kupiga simu kwenye nambari za huduma za kisheria zinazotumika jimboni kote 1-888-201-1014.